

TANGAZO LA SERIKALI Na. 323 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NYAMALEMBO YA MWAKA 2023

- Jina
1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Nyamalembo ya Mwaka 2023.
- Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355
2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.
- Mpango wa jumla na kina wa eneo
3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Geita.

—
JEDWALI
—

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira – nukta411456MS, 9681343KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa 103⁰ kwa umbali wa kilometa 0.76 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenyemajira – nukta 412203MS, 9681168KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa 163⁰ kwa umbali wa kilometa 0.72 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 412925MS, 9681211KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa 84⁰ kwa umbali wa kilometa 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta412839MS, 9681712KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa 88⁰ kwa umbali wa kilometa 0.27 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira- nukta 412568MS, 9681656KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa 169⁰ kwa umbali wa kilometa 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 411458MS, 9681653KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 127⁰ kwa umbali wa kilometa 0.37 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi